## CRP ina faida gani?

**Bili zisizohamishika, zilizopunguzwa**

CRP hutoa bili isiyohamishika ya kila mwezi kulingana na ukubwa wa boma na mapato au bili ya wastani. Haijalishi ni kiasi gani cha gesi unatumia, bili yako inakaa sawa mwaka mzima!

**Msamaha wa deni la zamani**

Ukiwa na deni ya zamani, PGW itaondoa sehemu ya deni hilo, kila wakati unapolipa bili yako ya kila mwezi. Katika muda wa miaka mitatu, unaweza kuondoa deni yote ya zamani.

**Mpango wa Faraja ya Nyumbani**

PGW inaweza kukupa huduma za bure za kunufaisha hali ya hewa kama vile kutengeneza hita za maji moto, au kubadilisha madirisha.

## Ninawezaje kudumisha ushirikiano na CRP?

Mara tu unapokubaliwa, lazima ufanye **yote** ya yafuatayo ili uendelee kuwa umesajiliwa:

- ◊ Lipa bili yako ya kila mwezi kikamilifu na kwa wakati
- ◊ Omba Programu Ya Nishati Ya Kusaidia Boma Zenye Upato Wa Chini (Low Income Home Energy Assistance Program, LIHEAP) (mpango wa usaidizi wa kupashiwa joto) kila mwaka na upe PGW ruzuku hiyo
- ◊ Fanya bidii kuhifadhi nishati
- ◊ Omba tena CRP kila mwaka au wakati ukubwa wa kaya/mapato yanabadilika
- ◊ Kubali huduma za kunufaisha hali ya hewa bila malipo, ikiwa zitatolewa.

## Wasiliana nasi

**Philadelphia Gas Works**

Idara ya Huduma kwa Wateja

Jumatatu hadi Ijumaa saa 8 a. m - 6:00 p.m

Nambari ya simu: 215-235-1000

## Vituo vya Huduma kwa Wateja

**Masaa**

9 a.m - 5 p.m

| **Makao** | **Siku imefunguliwa** |
|---|---|
| 4410 Frankford Ave. | Jumatatu, Jumanne, Alhamisi, Ijumaa |
| 212 W. Chelten Ave | Jumanne, Alhamisi, Ijumaa |
| 1337 W. Erie Ave. | Jumanne, Jumatano, Ijumaa |
| 1601 S. Broad St. | Jumatatu, Jumatano, Alhamisi |
| 5230 Chestnut St. | Jumatatu, Jumanne, Jumatano, Ijumaa |





# Mteja Wajibu Programu (CRP)

## CRP ni nini?

Programu ya Wajibu kwa Wateja (Customer Responsibility Program, CRP) ni mpango wa usaidizi ambao husaidia wateja wanaostahiki wenya kipato cha chini kumudu huduma ya gesi. Wateja hulipa bili ya kila mwezi ya kudumu-wakati mwingine huwa chini ya $25 kwa mwezi-kulingana na ukuwa wa boma na mapato, au bili ya wastani.

PGW



## Ninastahiki CRP?

Ikiwa wewe ni mteja katika maeneo ya makao— **mmiliki wa nyumba au mpangaji** —na unatimiza masharti yafuatayo ya mapato, unaweza kustahiki.

### 2020 Kiwango cha juu zaidi Mapato ya kila mwezi*

| Watu walio kwenye boma | Mapato ya juu zaidi ya kila mwezi |
|---|---|
| 1 | $1,610 |
| 2 | $2,178 |
| 3 | $2,745 |
| 4 | $3,313 |
| **Kila ya ziada** | **+$568** |


*Vikomo vya juu vya mapato ya kila mwezi vinategemea miongozo ya umasikini wa kitaifa, na hubadilika kila mwaka.

## Nitajisajili kuomba vipi?


### Hatua ya 1 Kusanya nyaraka

Lazima uwasilishe nakala zifuatazo **za kila mtu katika boma, pamoja na watoto.**

◊ **Kadi za usalama wa jamii**




◊ **Nakala za mapato kwa siku 30 zilizopita**
Mifano: Tiketi za kulipa; barua ya tuzo kutoka kwa Usimamizi wa Usalama wa Jamii kwa Usalama wa Jamii, Mapato ya Ziada ya Usalama (Supplemental Security Income, SSI), au nakala ya faida za Bima ya Usalama wa Jamii ya Ulemavu (Social Security Disability Insurance, SSDI); taarifa ya faida kutoka Idara ya Huduma za Binadamu au chapisho la My COMPASS; Nakala ya mafao ya ukosefu wa ajira; msaada kwa mtoto ulioamuriwa na korti, n.k
**Kurasa zote kutoka kwa nakala ya faida au mapato ya Usalama wa Jamii lazima zijumuishwe.**



Sample Company Name, Sample Company Address, 95220 — EARNINGS STATEMENT

| EMPLOYEE NAME | SOCIAL SEC.ID | EMPLOYEE ID | CHECK No. | PAY PERIOD | PAY DATE |
|---|---|---|---|---|---|
| James Robert | XXX-XX-6565 | 454545 | 259248 | 01/23/14-01/29/14 | 01/31/14 |

| INCOME | RATE | HOURS | CURRENT TOTAL | DEDUCTIONS | CURRENT TOTAL | YEAR-TO-DATE |
|---|---|---|---|---|---|---|
| GROSS WAGES | | | 1,000.00 | FICA MED TAX | 14.50 | 72.50 |
| | | | | FICA SS TAX | 62.00 | 310.00 |
| | | | | FED TAX | 159.50 | 797.48 |
| | | | | CA ST TAX | 44.26 | 221.31 |
| | | | | SDI | 10.00 | 50.00 |


| YTD GROSS | YTD DEDCTIONS | YTD NET PAY | TOTAL | DEDUCTIONS | NET PAY |
|---|---|---|---|---|---|
| 5,000.00 | 1,451.28 | 3,548.72 | 1,000.00 | 290.26 | 709.74 |

### Hatua ya 2 Fikia programu ya mtandaoni*

**Kujisajili ni kubofya tu!**

Nenda kwa www.pgworks.com/crp, chagua **Apply Now (Jisajili Sasa)**, kisha ingia au ujiandikishe kwa **My Account(Akaunti Yangu)** kufikia meneja wa akaunti ya mtandaoni ya PGW.




### Hatua ya 3 Chagua Jisajili kwa CRP*




Jibu maswali kadhaa kisha uwasilishe nyaraka zinazounga mkono. PGW itakutumia ujumbe mfupi au barua pepe sasisho kuhusu programu hii.

* Ikiwa huna namna ya kufikia mtandao, piga simu kwa 215-235-1000 kufanya ombi la CRP kwa barua, au tembelea Kituo cha Huduma kwa Wateja cha PGW.